**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**OFISI YA MKUU WA MKOA KILIMANJARO**

**MTIHANI WA PAMOJA WA MKOA KIDATO CHA KWANZA**

**021** **KISWAHILI**

**Masaa 2:30** **Novemba, 2025**

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina sehemu tatu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A,B na C.
3. Sehemu A ina alama kumi na tano(15), sehemu B ina alama sabini (70) na sehemu C ina Alama kumi na tano (15).
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na kila swali.
5. Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.
6. Vifaa vyote vya mawasiliano na visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha upimaji.
7. Andika jina lako katika kila ukurasa.
8. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi.

## SEHEMU A (ALAMA15)

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Nomino za Kiswahili zina makundi yake. Ipi kati ya hizi zifuatazo sio nomino ya dhahania?
A. Wema
B. Huzuni
C. Uongo
D. Askari

(ii) Katika kamusi, kidahizo pamoja na taarifa zake zote huitwa?
A. Sherehe ya kamusi
B. Matini ya kamusi
C. Kitomeo
D. Taarifa za kidahizo

(iii) Mapunda anataka kufahamu namna ya kuweka mkazo katika maneno ya lugha ya kiswahili yenye asili ya kibantu.Msaidie Mapunda kwa kuonesha namna mkazo unavyowekwa katika neno "Sanduku".
A. Sanduku'
B. Sa'nduku
C. 'sanduku
D. Sandu'ku

(iv) Tawi la sarufi linaloweza kurekebisha makosa ya lugha yaliyofanywa na mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili alieathiriwa na lugha mama.
A. Sintaksia
B. Semantiki
C. Fonolojia
D. Mofolojia

(v) Uanishaji wa aina za maneno huzingatia dhima ya kila neno. Ni neno gani ambalo haliwezi kusimama pamoja na nomino?
A. Kiwakilishi
B. Kielezi
C. Kivumishi
D. Kiunganishi

(vi) Mwalimu alimwomba Kidana afafanue maana ya lugha kisha Kidana akasema ni "**t**hauti cha na**t**hibu". Mwalimu alifurahi na kusema hongera kaka wa kipare unafikiri mwalimu alimwambia Kidana ni mpare kwa sababu gani?
A. Lahaja
B. Lafudhi
C. Kiimbo
D. Mkazo

(vii) Silabi ni fungu la sauti linalotamkika mara moja katika sentensi ifuatayo neno lililopigiwa mstari lina silabi ngapi? “Mtoto anakimbia vizuri”.

A. Tano
B. Tatu
C. Mbili
D. Moja

(viii) Yafuatayo ni matumizi ya alama ya mkato(,) isipokuwa

A. Kuweka pumziko fupi katika sentensi
B. Kutenga maneno yaliyo katika orodha
C. Kuashiria maneno ya msemaji
D. Kuonesha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume

(ix) Lugha hujengwa na

A. Herufi, Silabi, Sentensi, tukio na maneno
B. Sauti, Silabi, neno na tungo
C. Mtu au Kikundi cha watu peke yake
D. Msemaji na msikilizaji

(x) Mama alikuwa nyumbani. Neno “alikuwa” ni aina gani ya neno?

A. Kitenzi kikuu
B. Kitenzi kishirikishi
C. Kitenzi kisaidizi
D. Kiunganishi

Majibu

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha sentensi zenye matumizi ya viwakilishi katika ORODHA A na aina ya kiwakilishi husika kutoka ORODHA B kwa kuandika jibu sahihi.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) Ameleta chetu<br>(ii) Wangapi wamehesabiwa?<br>(iii) Shujaa amepewa zawadi<br>(iv) Wale hawafanyi mazoezi<br>(v) Mtoto anaomba chochote ale. | A. Kiwakilishi cha sifa<br>B. Kiwakilishi kimilikishi<br>C. Kiwakilishi cha taarifa<br>D. Kiwakilishi cha kuuliza<br>E. Kiwakilishi cha a- unganifu<br>F. Kiwakilishi cha idadi<br>G. Kiwakilishi cha kioneshi<br>H. Kiwakilishi cha pekee. |

Majibu:

| OORODHA A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| ORODHA B | | | | | |

SEHEMU B (ALAMA 70)

3. Eleza fasili ya maneno yafuatayo.
   (i) Lugha……………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………....
   (ii) Nomino…………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
   (iii) Tafsida…………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
   (iv) Mawasiliano…………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
   (v) Kamusi…………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………

4. Taja umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili katika maendeleo ya nchi yetu. (Toa hoja tano (05))
   (i) ……………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………….......
   (ii) ……………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………….
   (iii) ……………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………….
   (iv) ……………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………….
   (v) ……………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………….

5. (a) Ukiwa ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza umejifunza aina za maneno ya Kiswahili badili vitenzi vifuatavyo kuwa nomino.
   (i) Toroka……………………………………………………………………………

(ii) Imba……………………………………………………………………………..
(iii) Tangaza…………………………………………………………………………….
(iv) Kufa……………………………………………………………………………..
(v) Kula……………………………………………………………………………..

(b) maneno katika lugha yana dhima mbalimbali, bainisha aina za maneno yaliyopigiwa mstari.

(i) Ng'ombe amepotea jana………………………………………..
(ii) Nyumba yetu ni ndogo sana……………………………………..
(iii) Yule ni mwizi………………………………………………….
(iv) Mjomba mrefu amesafiri………………………………………
(v) Kaka na dada wanafua nguo…………………………………….

6. (a) Nini maana ya kiimbo…………………………………………………………......
…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(b) Matumizi ya kiimbo husaidia kubainisha lengo la mzungumzaji. Fafanua malengo ya mzungumzaji katika sentensi zifuatazo.

(i) Kaka analima kwa bidii…………………………………………………….
(ii) Kaka, lima kwa bidii……………………………………………………….
(iii) Kaka analima kwa bidii?………………………………………………….
(iv) Juma analima kwa bidii!.........................................................................................

7. Eleza sifa tano (05) za lugha ya mazungumzo.

(i) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
(ii) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
(iii) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
(iv) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
(v) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

8. Neema amekuwa haelewi kwanini picha na michorovipo kwenye kamusi? Wewe kama mwanafunzi wa kidato cha kwanza mweleze kwa hoja tano (05) kwanini picha na michoro hiyo ipo kwenye kamusi?

(i) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
(ii) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
(iii) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
(iv) …………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

(v) ………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

9. Taja mambo matano (05) ya kuzingatia wakati wa kusikiliza mazungumzo.
   (i) ………………………………………………………………………………
   (ii) ………………………………………………………………………………
   (iii) ………………………………………………………………………………
   (iv) ………………………………………………………………………………
   (v) ……………………………………………………………………………..

**SEHEMU C (ALAMA 15)**

10. Umechaguliwa kushiriki katika mashindano ya uandishi wa insha ngazi ya Taifa yatakayofanyika mkoani Mbeya tarehe 10 disemba wakati wa likizo. Andika barua kwa mzazi wako kumtaarifu kuwa hutorejea nyumbani bali utaenda kushiriki katika mashindano hayo. Jina lako liwe Ayubu Juma.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…..
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………